USHUHUDA

Ndugu Don, asante, Huu ni mshangao wa ghafla. [Mtu fulani anasema "Mzuri."—Mh.] Naam, ni . . . ["Amina."] Asante, yeyote aliyesema hivyo. ["Nilisema."] Asante, sana.

2 Nilikuwa nikizifurahia hizo nyimbo. Jamani, napenda kuzisikia hizo! Mnajua, napenda uimbaji mzuri, na huwa nausikia kwa wingi ninapofika hapa. Kwa kawaida mimi si . . . Wakati ninapofika, nikiwa na ibada za uponyaji ama nyinginezo, huwa inanibidi kukaa peke yangu, binafsi, na ndipo vijana huzipata hizi kanda. Kisha wakati ninapofika nyumbani, au ninapokuwa na kazi za kufanya ofisini, ndipo huwa nakaa chini na kuzisikiliza hizo kanda, tena na tena. Na huwa nasikia kila kitu kilichosemwa.

3 Nami nina furaha kumwona Ndugu Gerholtzer hapa asubuhi ya leo, rafiki wa kale wa Injili, kwa miaka mingi iliyopita alikuwa nje katika kazi hii hii, akiwaombea wagonjwa, labda miaka mingi kabla sijawahi kujua kuhusu kuombea wagonjwa. Na kwa hiyo, na watu wengine hapa, rafiki zangu binafsi. Nimeona umati mkubwa hapa usiku uliopita kutoka katika Maskani ya Jeffersonville. Na kwa hiyo tunafurahi sana.

4 Nami nilikutana na Ndugu Young Brown. Nilisema, "Ndugu Jack alisema jina lake lilikuwa 'Young,' na linamfaa." Wakati aliponiambia alikuwa na umri wa miaka sitini na kitu, ilikuwa vigumu kwangu kuamini hilo. Hajabadilika hata kidogo tangu mara ya kwanza hapa Shreveport. Hiyo ni kweli, anaonekana vile vile tu.

5 Vema, Mungu ni mwema kwetu sisi. Na mimi—mimi napenda hizo, jinsi zile nyimbo asubuhi ya leo, zina—zina kina chake; kitu halisi, kitu ambacho—ambacho—ambacho kina maana fulani. Unaweza kuzisikia kwa furaha. I—ilikuwa vigumu kujizuia kulia kwa sauti, wakati nilipowasikia wao wakiimba ule wimbo, kuhusiana na Zaburi 23 hapo. Na kisha—kisha ukafuata, na huu wimbo mzuri ambao wameuimba hivi sasa, wale watatu pale. Kufikiri tu jinsi . . .

6 Kuna kitu ndani yake, ambacho unakihisi ndani yako, mwamsho wako ukidunda-dunda, kujua kwamba Ufalme wa Mungu umekaribia. Mambo haya ambayo tumezungumza habari zake na kuyastaajabia, sasa yako karibu kutokea. Baadhi yetu huenda wakalala kabla ya wakati huo kufika, lakini hilo halituzuii kufufuka kwetu, kwa sababu, linatupea yale—yale majaliwa ya kuja kabla ya wale waliobadilika.

7 "Parapanda ya Mungu italia; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza; kisha sisi tulio hai, tuliosalia." Je umeona utaratibu wa kufufuliwa? "Tutanyakuliwa pamoja

nao." Tunakutana sisi kwa sisi kabla hatujakutana na Yeye. "Tutanyakuliwa pamoja tukutane nao. . .pamoja nao, ili tumlaki Bwana hewani."

8 Unaona, Yeye ni Mungu, na ndipo wakati Yeye anataka kuabudiwa, hiyo ndiyo asili Yake halisi, ni kuabudiwa, kwa sababu Yeye ni Mungu. Na Yeye anajua kama tungekuwa kule, tungekuwa tunachungulia kando kwa macho yetu, kuona kama yule mwingine yuko, bali, na ndipo isingekuwa njia kamili ya kuabudu kwa uhuru. Wakati tutakaposimama kule, na—na tunajua tumekwisha kutana kwanza, na tumekwisha salimiana sisi kwa sisi, na ndipo tumesimama karibu na Yeye Yule aliyesababisha yote haya, na kuimba nyimbo za ukombozi! Kama Ndugu Jack alivyotoa matamshi mara nyingi, "Malaika watakapoizunguka dunia, huku wameinamisha vichwa vyao, bila kujua tunazungumza nini." Unaona, kwa sababu hawajawahi kukombolewa. Bali ilipasa sisi tukombolewe, na hivyo sisi tutamvika Yeye taji kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.

9 Sijui niseme nini. Sikuwaza kuzungumza lolote; nimekuja tu hapa. Nadhani ni wakati wa ushuhuda, kutoa tu ushuhuda. Na hivyo, usiku huu, Bwana akipenda, nafikiri. . .Nimetazama katika ile ratiba ndogo, nami. . .kwa ajili ya—ya ibada, nami nafikiri yanibidi kuleta ujumbe wangu usiku huu, juu ya Pasaka au, samahani, ujumbe wa Shukrani usiku huu. Na kisha tunataka kuchukua wakati huo, labda siku zilizosalia za juma, kama Bwana akipenda, kuwaombea wagonjwa. Tunataka nyinyi mkusanyike, baada ya hii sikukuu ya Shukrani, ambayo ni ya ukumbusho wa mkutano mkubwa uliofanyika wakati mmoja hapa Shreveport, kidogo. . .yapata miaka mitatu iliyopita, wakati mlipopata huu ufunuo wa kukusanyika. Na Bwana aliwabariki mno hapa katika mkutano huo! Na mimi—mimi nasadiki kwamba Bwana ataendelea, na ataziokoa roho za watu hapa hadi jina la mwisho limo katika Kitabu katika kituo kikuu cha kumbukumbu za Mungu huko Juu, wale ambao wamemkubali Kristo kuwa Mwokozi, waliojazwa Roho Wake.

10 Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa kitambo kidogo. Ninawaza juu ya Andiko hapa.

11 Bwana Yesu, tu watu wenye shukrani sana asubuhi ya leo, lakini hata hivyo hatuna maneno ya kutosha. Kama mioyo yetu ingetoa nafasi kwa lile sisi—lile sisi tunataka, hatujui jinsi gani sisi wenyewe tungeenenda. Na hapo, si ajabu, Wewe ulisema, "Haitakuwepo nafasi ya kutosha kupokea baraka ambazo Mungu angetumwagia sisi." Na sisi tunashukuru kwa ajili ya jambo hili. Nasi tunaomba Bwana, tunapoinamisha vichwa vyetu kukusujudia Wewe, kwamba Wewe utapokea shukrani zetu. Kuna mambo mengi mno ambayo yatupasa kuyatolea shukrani, na hatungeweza kuyatamka, ila tu twasema, "Mungu ashukuriwe!"

12 Na zaidi ya mambo yote ambayo tunayatolea shukrani, ni hiyo Karama kuu ya Mungu kwa ulimwengu, wakati Mungu alipomtoa Mwanawe, kutengeneza njia ya ukombozi wetu. Sisi tu wenye shukrani mno kwa ajili ya Hiyo! Nasi tunaikumbatia Hiyo, na tumefanya hivyo tangu. . .Bwana, ninaweza kukumbuka, tangu nilipokuwa mvulana mdogo, nimeishi kwa ajili ya Hiyo. Na sasa ninapozeeka, najua kwamba jua litatua tu siyo mara nyingi zaidi, hata nitakapoitwa, na, yale niliyoishi kwa ajili yake, nitakwenda kuyafurahia. Najua, Bwana, kwamba wapo wenzangu wengi raia wa Ufalme ule ule, ambao wanangojea vivyo hivyo, asubuhi ya leo, wakati huo ufike. Kwa kuwa, jambo lile ambalo tumelifungia safari, kumtumikia Yeye na kujaribu kuwaongoza wenzetu kwenye Uzima wa Milele, hiyo saa kuu punde inakaribia. Tunaweza kuihisi kidogo ndani yetu, kwamba iko—iko karibu zaidi kuliko labda tunavyoweza kufikiri.

13 Nasi tunaomba kwamba Wewe utatubariki sasa, na kuendelea na baraka Zako ambazo Wewe umekuwa ukitupa asubuhi ya leo. Na sasa tunaposoma sehemu ya Neno Lako, ama aya moja au mbili, tunaomba kwamba Roho Mtakatifu aliye mkuu atazichukua aya hizi, na ushuhuda, kwa utukufu Wake. Katika Jina la Yesu twaomba. Amina.

14 Niliwaza juu ya sehemu fulani hapa, naamini inapatikana katika—katika Wakorintho, 2 Wakorintho 9, aya ya 14, na ya 15.

> *. . .wakiomba dua kwa ajili yenu, wawaonea shauku kwa. . .neema ya Mungu iliyozidi sana ndani yenu.*
>
> *Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo.*

15 Paulo, hapa anazungumza juu ya neema ya Mungu iliyo ndani yenu, Kipawa tusichoweza kukisifu kama ipasavyo, cha Roho Mtakatifu, ambaye anakaa miongoni mwa watu. Alikuwa akimshukuru Mungu kwa ajili ya kile walichokuwa nacho, Roho Mtakatifu alikuwa amekuja juu ya hawa watu, Kipawa cha Mungu tusichoweza kukisifu kama ipasavyo, cha thamani mno na kisafi.

16 Sasa, mimi—mimi sina kitu chochote akilini mwangu, hasa, hivyo niliwaza kuwa ningetoa ushuhuda kidogo wa ujuzi wangu wa Kristo katika siku chache zilizopita. Umekuwa wenye utukufu sana.

17 Maisha yangu yote, nyinyi mnayafahamu. Nyinyi mmenisikia mimi, wengi wenu. Nami niliwaza kuwa ningalisema jambo hili kwa ajili ya baadhi ya watu wa Maskani ambao wamekaa hapa. Kule. . .Kusanyiko langu kule Maskanini linayo yapata mataifa matatu, asubuhi, wakati tunapozungumza; Mexico, Canada, na Marekani. Karibu kila. . .Hapa hivi majuzi kulikuwa na majimbo ishirini na manane, kwa ibada moja ndogo ya shule ya Jumapili, unaona, majimbo ishirini na manane

mbalimbali yaliwakilishwa. Nataka kusema hili kwa utukufu wa Mungu. Katika kusafiri, nafikiri kwamba. . .Kwa njia ya maombi na dua, tukiwa wale waliokataliwa kama tulivyokuwa sisi, tumekataliwa na kanisa la ulimwengu, kama wanavyojiita leo, kwamba Maskani imekua mpaka kuwa makao makuu ya uweza mkuu wa neema ya Mungu, kuliko mahali popote ninapojua ulimwenguni. Sijawahi kuona mambo kama hayo, yale anayoyatenda Bwana kule. Hatuna uwezo wa kusifu, jinsi, ambavyo Yeye anatenda kule, katika unyenyekevu tu, watu wakija tu kutoka kila mahali. Nasi tumeshukuru kwa ajili ya hicho kituo kidogo, mahali ambapo baadhi ya watu nchini hukusanyika kufurahia ile neema, na—na kueneza neema kwa wengine.

18 Sasa, maishani mwangu mwote, ilionekana kuwa nilipendelea kwenda upande wa Magharibi. Na wengi wenu mmesoma hizo habari na kusikia kanda.

19 Huduma ya kanda ni ya ulimwengu wote, kila mahali. Nafikiri ni njia moja aliyo nayo Mungu kusambaza Ujumbe katika nchi za makafiri, kule ambako yabidi zitafsiriwe. Na kule Ujerumani, na kwingineko, wanazo kanda zinazopelekwa katika makusanyiko yao, ya mamia na mamia ya watu; nao hutia vitu vidogo katika masikio yao, na kuvichomeka katika kinasasauti. Na jinsi tu ninavyozungumza, mhudumu husimama huko akizungumza vile vile, na katika lugha zingine, na kuuleta mbele ya mamia ya watu. Na mamia ya watu wanaokolewa na kuponywa, kupitia tu kanda zinazosambazwa kote ulimwenguni. Zote katika Kiingereza, lakini zikitafsiriwa katika lugha nyingi, nyingi sana za makabila kote ulimwenguni. Wao wanatupasha habari, kwa njia ya barua.

20 Na sasa nasema hili, itakuwa ushuhuda wa binafsi kwa utukufu wa Mungu, ili kwamba mpate kuelewa katika usiku wa siku zinazofuata, yale ninayotaka kusema, kama Bwana akipenda. Mtaelewa. Kama nilivyokuwa najaribu kusema usiku uliopita, ulimwengu unafikia mahali ambapo unaanguka, kisiasa, kijamii, kiuchumi.

Mnasema, "Uchumi? Fedha zaidi!"

21 Ndiyo, lakini zinatoka wapi? Tumekopeshwa kutokana na kodi ambazo zitalipwa miaka arobaini ijayo tangu leo. Halina hela. Limefilisika, taifa, siyo taifa hili, bali yote. Na hakuna njia ya kuliimarisha tena. Na huo ni mtego hasa umetegwa kulinasa taifa hili katika jambo fulani. Nanyi nyote mna busara juu ya jambo hilo. Naam, ni nani aliye na utajiri wa ulimwengu? Ni nani unaushikilia? [Mtu mmoja anasema "Rumi"—Mh.] Hakika, inaushikilia. Rumi inaushikilia. Na tunapofanya hivyo, tunapofilisika, badala ya hawa wafanya biashara wakubwa kuimarisha mvinyo, na kadhalika, kama vile. . .Lazima fedha zipatikane; tutakacholazimika kufanya, ni ama kubadilisha

fedha au kukopa fedha. Na watakapofanya hivyo, itakuwa ni kuuza haki ya mzaliwa wa kwanza, hasa, kikamilifu tu, na ndivyo Maandiko yanenavyo kuhusu jambo hilo.

22 Ningependa kupata mahali fulani wakati fulani, Bwana akipenda, wakati hema litakapoonekana. Nami naamini kwamba ni hivi karibuni sasa, hivi karibuni nitazuru ulimwengu mzima. Ninayo mikutano ya ulimwenguni kote inayokuja sasa. Nami ningependa kupata mahali ambapo ningeweza kukaa chini kwa karibu majuma sita, na kuyachukua mambo hayo tu na kuyapitia, mnaona, huku na huko, kupitia katika Maandiko.

23 Na inastaajabisha kuona saa ambayo tunaishi! Inaniogopesha mimi. Inaniogopesha mimi, siyo kwa sababu . . . Moyoni mwangu kengele za shangwe zinalia, kujua kwamba Kuja kwa Bwana kumekaribia mno. Lakini, kinachoniogopesha mimi, ni kujua kwamba wengi mno hawako tayari kwa ajili ya hii saa iliyo mbele yetu. Ubaya ndio huo.

24 Ni wangapi waliwahi kusikia kisa cha wale kindi kule juu wakati ule? Wengi, loo, bila shaka, nakisia, kila mahali. Jambo dogo kama hilo lilitokea hivi majuzi. Nami nilikuwa . . . Mmesikia kile kisa kuhusu ile milima, nikishuka chini, wakati Bwana alipoandika mambo hayo juu ya milima hivi majuzi. Jamani, maisha yangu . . .

25 Mimi si mhubiri. Kila mtu anajua hilo. Mimi si mhubiri. Lakini imefanyika kwa—kwa jinsi ya kiroho, ya—ya kutazama mambo na kuona mambo yakitendeka, na kuwaonya awali watu juu ya mambo yatakayotokea. Na hayo ndiyo maumbile yangu. Siwezi kujizuia, kama vile tu wewe usivyoweza kufanya lolote juu ya maumbile yako. Lakini Mungu ametuweka sisi, kila mmoja, katika ule Mwili, kutenda mambo fulani. Nami natazama kila tendo dogo, kila kusudi, kila nia, kwa sababu kila kitu kinatawaliwa na . . . kinatawaliwa na roho.

26 Kanisa hili liliwekwa hapa kwa madhumuni fulani. Kuna roho fulani nyuma ya kanisa hili. Hakika. Kuna roho nyuma ya nyumba yako, nyuma ya kila jengo. Nyuma ya kila kitu kuna roho, kusudi, na nia. Kanisa hili likija hapa kutukuza sana namna fulani ya utaratibu wa kibinadamu ama kitu kingine, ndipo kusudi lake si sahihi; bali kama limewekwa hapa kujaribu kufanikisha kitu fulani kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, ndipo kusudi lake na nia yake, vyote viwili, ni sahihi, kama kusudi limeelekezwa hivyo.

27 Sasa, nimekuwa nikiwaza. Tangu ile huduma, kiwango cha kwanza, cha pili, na cha tatu cha huduma. Wakati nilipokuja kwa mara ya kwanza Shreveport, niliwaambia nyinyi watu kwamba Bwana . . . ungelaza mikono yako juu, kama vile juu ya mkono wangu, na ungetoa ishara ile ile. Na Roho Mtakatifu hakukosea hata mara moja, bali aliwaambia hasa matatizo mliyokuwa nayo. Ndipo niliwaambia wakati huo, hayo. Yeye

aliniambia mimi siku hiyo, kwamba, “Wakati unakuja ambapo utajua siri za moyo,” bila kujua kwamba Neno linasema hayo yatatokea. Sikujua hilo. Lakini Neno linasema kwamba, “Neno la Mungu huyatambua mawazo na makusudi ya moyo,” Waebrania, sura ya 4.

28 Sasa, hilo Neno, unaona, kamwe usiliache hilo Neno. Lazima udumu hasa na hilo Neno, jinsi Neno lilivyoandikwa. Usiweke tafsiri yako ya binafsi juu Yake. Liseme tu jinsi lilivyoandikwa. Hilo ni Neno la Mungu, na huyo ni Mungu. Mungu na Neno Lake ni sawa, sawa tu.

29 Na kama nilivyosema usiku uliopita, kuna sehemu ya Neno iliyowekwa kwa kila wakati. Na kuna upako unaoshuka, ambao unaleta hiyo sehemu ya Neno kwa wakati ule. Na mnaona mahali tulipo leo. Someni ni nini tunapaswa kuwa tukitenda, ndipo mtajua tumefika wapi. Ninaona tu jambo moja limebaki, kule kuja kwa Bwana Yesu, wakati wowote, Kunyakuliwa kwa Kanisa nasi tutamlaki hewani. Sasa mambo haya yapasa yatimie katika siku hizi, jinsi tu Yeye alivyoahidi kwamba angefanya.

30 Na sasa yapata miaka mitano iliyopita, baada ya hiyo kumaliza wakati wake. Kila kimoja cha viwango hivyo kilikuwa kimemaliza wakati wake. Na Yeye alitoa maono, na wengi wenu wasikilizaji wa kanda na wengineo, mnajua kwamba kiwango kimoja zaidi kingekuja, na Yeye alichora hicho kikamilifu mno. Kuna mtu anayekaa papa hapa sasa, ninamtazama, alikuwapo pale na aliona hayo yakitokea kwa ukamilifu tu kama nilivyowahi kuona katika maisha yangu. Na hata alipiga picha Yake, ya kile Bwana Mungu alichosema kwamba kingetokea. Nasi tulikwenda pale pale, na hapo Hilo lilitokea, vile vile tu na alivyonena. Yapata tu . . .

31 Kama la Machi 17, toleo la Machi la gazeti la *Life*, mmeona hiyo duara ya Nuru angani, maili therathini kwenda juu, upana wa maili ishirini na saba. Mbona, mvuke unakaa yapata maili tisa tu kwenda juu, na hata hawawezi kujua ilikuwa kitu gani.

32 Na hapo akisimama chini yake, kuna mtu ambaye ameketi hapa hivi sasa, alikuwa amesimama pale karibu nami, wakati Malaika saba walishuka chini kutoka kwa Mungu, wakionekana wazi wamesimama pale, na wakaniambia kuhusu wakati wa mwisho, na funuo hizi na mambo ya Kitabu cha Ufunuo, zile Muhuri Saba, na walisema, “Rudi nyumbani, na mmoja baada ya mwingine tutaleta Ujumbe.” Hiyo, hiyo ni kweli. Nalo lilipanda juu, na likaanza kugeuka jeupe lilipokuwa likipanda juu, likiendelea juu; na mlipuko ukatikisa milima, hata mawe, ukubwa wa—wa—wa ndoo, yalianguka kutoka milimani, namna hiyo.

33 Na hapakuwa na cho chote karibu. Hata magazeti yalisema walikagua kuona kama kulikuwa na kizuio cha sauti, au ndege, ama kitu kingine. Hapakuwa na cho chote, hazikuwako ndege

kule juu, hapakuwa na cho chote. Hata hivyo, ndege ingurumayo haingeweza kufanya hivyo.

34 Na kisha jambo hilo lilitabiriwa kwamba lingetokea hivyo, miezi sita kabla halijatendeka, miezi sita. Na lilitokea basi. Na Sayansi wanalichunguza leo, kule Tucson na sehemu mbalimbali, hawawezi kuelewa kitu gani kilikuwa kule juu. Na ndipo mkipata lile gazeti na kuangalia, mnaweza kuona hata maumbo ya mbawa Zao bado yako pale huku wakipaa kwenda juu, wale Malaika saba. Nasi tunajua kwamba mambo haya ni sahihi, marafiki. Loo, kama kuna wakati ambapo kanisa lapaswa kuwa na uaminifu sana, yapasa iwe ni sasa hivi. Sasa!

35 Lakini sasa, limefanya kitu fulani kwangu, ndani yangu. Kwa miaka mitano sasa, nimekuwa nashangaa kuna kasoro gani. Nilijisikia moyoni mwangu kama nilikuwa—nilikuwa nimesetwa na kitu fulani, nami—nami, sikuweza kujua ilikuwa ni kitu gani. Katika kipindi cha huu mseto mkuu, na kadhalika, niliyumbayumba huku na huku, kote nchini.

36 Na serikali ilikuwa ikinifanyia upelelezi kwa sababu, wakati tunafanya mikutano, mtu anaandika hundi "William Branham" nami huitia sahihi na kuirudisha. Na ndipo tulikuwa na fungu la mikutano yetu yo—yote, nao walipochunguza waligundua kwamba zilitumiwa kulipia gharama za mikutano. Hata hivyo, kwa vile niliandika jina langu mle, nilijitambulisha kuwa hiyo hundi ni yangu, na wakanishtaki mimi kuwa "nadaiwa na serikali dola laki tatu." Nao hawakuniachilia niondoke, nami ilinilazimu kukaa hapa, na kadhalika, kwa mda mrefu haya yote yapate kuchunguzwa. Na—na mimi siyo, kila kitu kilikwenda. . . Wao walisema, "Ndiyo, ziligharimia mikutano, lakini watu walikuandikia wewe hundi. Na wakati ulipoitia sahihi, ulijitambulisha na hiyo hundi, na unadaiwa kodi yake. Hata kama ungeishika kwa sekunde moja, ingekuwa bado ni yako kwa sababu wewe uliitia sahihi."

37 Mimi sikujua jambo hilo. Mimi sina ujuzi wo wote wa hizi sheria na mambo kama hayo. Nilipaswa kuwa na mhuri nipate kuipiga mhuri, badala ya kuitia sahihi. Wakati nilipoitia sahihi, ilimaanisha ni yangu. Na ndipo waliangalia katika fungu hilo na kugundua, humo, kuwa ziliwekwa katika ile hazina na kutumika hivyo. Napata mshahara kutoka katika kanisa langu, dola mia moja kwa juma. Kuna mdhamini ambaye ameketi pale, amekaa pale, ambaye anajua kwamba hiyo ni kweli. Na ni hizo tu ninazopata kutoka humo. Na, la sivyo, zinatumiwa kugharimia mikutano.

38 Sasa, nilijisikia kama nimesetwa, kwa miaka minne au mitano iliyopita. Naam, nilikuwa nimekwenda Canada, hivi karibuni, katika ziara ndogo ya kuwinda. Na nilipofanya hivyo, Bwana alinisaidia kule nikaliongoza kabila lote la Wahindi kwa Bwana Yesu. Na itanibidi kurudi kule wakati wa—wakati wa—

ghuba litakapoyeyuka barafu, juu kule, na kadhalika, kubatiza kabila lote, katika Jina la Bwana Yesu; kwa sababu ya kuponywa kwa mwanamke Mhindi aliyekuwa anakufa kwa ugonjwa wa moyo, ambaye kasisi hakumwendea, kule ndani ya misitu ambako ilinibidi kusafiri kwa saa nyingi, juu ya farasi. Kuna watu ambao wanaketi hapa sasa, waliokuwepo wakati jambo hili lilipotendeka.

39 Na sasa, basi, nilipokuwa nikiteremka, ilinibidi kusimama Colorado, kuwatembelea baadhi ya marafiki wangu kule, wahudumu. Mimi ni—mimi ni mwongozaji wa wawindaji katika Colorado, na nilikuwa nawapeleka katika msafara wa kuwinda. Wawili au watatu kati ya watu hao, watatu ama wanne, watano wao wameketi hapa hivi sasa kujua jambo hili. Na kulikuwa na ukame sana kule Colorado mwaka huu, kama ilivyokuwa nchini kote. Na mioto ilikuwa hasa . . . inakwenda kuwa mibaya hasa, hivyo walicheleweshа kidogo kipindi cha kuwinda.

40 Lakini wakati tulipokuwa juu kule, zilitolewa habari kwamba—kwamba tufani ya theluji inakuja. Na ni hatari kuwa milimani wakati huo, kwa sababu mara nyingine nimeona kuwa huwezi hata kuona mkono wako mbele yako, kwa masaa mengi sana, na futi thelathini za theluji zinaanguka ghafla wakati mmoja, katika muda wa masaa machache, inafunika, na unaangamizwa. Kwa hiyo nikawaambia ndugu zangu, asubuhi hiyo tulipokuwa tunaondoka, nilisema, "Sasa tufani ya theluji . . . "

41 Yapata watu mia moja, au zaidi, walikuwa nyuma yetu. Na huku yanakuja magari madogo, malori, na mengineyo yalikuwa yanatoka, kwa sababu walikuwa wanajua jambo gani litakalotendeka. Hakuna hata mmoja aliyeachwa nyuma, isipokuwa mchungaji wa ng'ombe peke yake huko, ambaye, anakaa huko majira ya kipupwe.

42 Na sisi tulikuwa ndio pekee, gari pekee, tulibaki huko. Nami niliwauliza wale ndugu. Nao walisema, "Tutabaki." Kwa hiyo basi, "Vema," nilisema, "sasa muwe tayari." Nasi tulikwenda nje na kuchukua . . . mhudumu wa Kimethodisti na mimi tulikwenda tukachukua mikate zaidi na vyakula vingine, hivyo tuliweza kupata; ilikuwa yapata maili thelathini kwenda na kurudi. Hivyo basi tulirudi, Ndugu John na wengine wao wakikaa hapa, waliisikia hiyo na wakaondoka; waliondoka kule wakati ule, kisha tufani ya theluji ikavuma. Basi sisi tungebakia huko, nami nilikuwa nakwenda mkutanoni kule Tucson na nikampigia mke wangu simu na kumwambia kwamba tunge . . . kama sikufika kule, amwambie mtu mwingine apachukue mahali pangu.

43 Na kesho yake asubuhi tulianza safari. Nilisema "Sasa, mara ya kwanza," kulikuwa na mawingu mazito, "mtakaposikia mvua ikinyesha, ama lolote, rudini kambini haraka mwezavyo, kwa sababu katika muda wa dakika kumi, dakika kumi na tano hivi,

kamwe hamtaona njia ya kurudi." Na hivyo ilinibidi kuwapanga wale watu, na walikwenda juu ya kile kilele, wakitembea huko, wakijaribu kuwafukuza kulungu kusudi wateremke.

44 Na nilikuwa, siku chache kabla ya wakati huo, nikifyatua bunduki yangu, kule Tucson; niliporudi kule nikaielekeza kidogo mkono wa kulia. Nilimpiga risasi kulungu dume mkubwa ambaye nilikuwa nimemtafuta kwa miaka mingi, na risasi ilimpiga juu sana, naye alifia kule chini hata sikuweza kumpata, hali ya hewa ilikuwa inaanza kuwa mbaya.

45 Niliwaza, "Nitakimbilia kule niangalie." Na nilipofika kule juu ya mlima, niliona mvua ikianza, mvua ya theluji ikianguka, na matone makubwa ya theluji, ukubwa wa sarafu ya dola, yalitiririka kila mahali, na pepo zikivuma. Nilijua kuwa kila mtu alikuwa anakimbia, kurudi kwenye kambi wakati huo. Naam, nilisubiri muda kidogo, na niliwaza, "Sitaweza kumpata huyu kulungu kwa wakati huu, katika dhoruba hii."

46 Hivyo tuliendelea kwenda, tulianza kuteremka mlima, niliweza kuona yapata umbali wa futi kumi tu mbele yangu. Na yapata . . . Nilikuwa yapata maili nne au zaidi, kufika mahali pale. Nilijua, niliteremka mlima, nikiijua ile nchi vema, kwa sababu nilikuwa nikichunga ng'ombe kule kwa miaka na miaka. Nilipokuwa nateremka mlima, yapata nusu maili kutoka kwenye safu ya huo mlima, mahali ambapo unapita *hivi* nyanda za juu mahali nilipokuwa. Na hapo kulikuwa . . .

47 Nilikuwa nahisi hiyo simanzi ya kutisha. "Nimelia. Nimeomba. Nimekiri. Nifanyeje? Nimefanya nini?" Ni kama kwamba umetenda jambo ovu sana, kana kwamba umemuudhi mtu fulani, na unajua kuwa unapaswa kulirekebisha jambo hilo. Kitu gani kilikuwa kinanihukumu? Sikujua. Nilisema, "Bwana, ikiwa Wewe utanifunulia tu jambo hili, nitalirekebisha. Lakini nimefanya nini isipokuwa kusimama na kuhubiri, na kutenda kila ninalolijua? Na nimejaribu kuishi bila mawaa, bila hitilafu, na kulingana na Maneno Yako tu. Lakini nimefanya nini?" Na hata hivyo hiyo simanzi haikuniondoka, mwaka baada ya mwaka. Niliwaza kuhusu jambo hilo kule mlimani, asubuhi hiyo, na nilianza kuteremka.

48 Jana yake ilikuwa sikukuu yangu, pia, mimi na mke wangu tulioana miaka ishirini iliyopita siku hiyo. Na sijawahi kuwa nyumbani katika sikukuu yetu. Na siku zote huwa nakwenda kule mlimani, mahali padogo palipo na vifutu watetemekao. Mwaka wa kwanza tulipooana, sikuwa na fedha za kutosha kwenda katika fungate, kwa ziara ndogo, na kisha kufanya ziara ya kuwinda pia, kwa hiyo nilimpeleka mke wangu katika ziara ya kuwinda badala ya fungate. Hivyo ilionekana kama, tuliyapata, kupata yote mawili kwa wakati mmoja.

49 Nami nakumbuka, jamaa ndogo, mimi—mimi nilimchukua na kumrusha juu ya magogo, na kadhalika. Na tulifika mahali

padogo, na nikampiga picha, na siku zote yaonekana kuwa—yaonekana kuwa nzuri. Huwa naiwaza hiyo, na nawaza kuhusu nywele zake nyeusi na jinsi alivyokuwa mzuri; na sasa ana mvi na jinsi alivyobadilika katika muda wa miaka michache.

50 Nikawaza, "Naamini nitapanda kwenda kule, bali ni—ni vigumu sana." Theluji ilikuwa gumu sana wakati huo.

51 Nilijua kuwa ilinipasa kuingia, kwa sababu walikuwa wametangaza, "Tufani kubwa ya theluji inakuja!" Walikuwa wameitangaza kwa taifa zima. Sijui iwapo Tom Simpson yuko hapa asubuhi ya leo, au la. Akija kutoka Canada, aliambiwa na redio, hata asipitie katika ile nchi. Kila mtu alisema, "Usipitie huko. Pitia njia nyingine, kwa sababu tufani ya theluji ya kutisha inakumba kila mahali."

52 Na nilianza kuteremka mlima, nikiwaza jambo hilo, na ilikuwa yapata saa nne asubuhi. Na kwa ghafla, wazi wazi tu kama mnavyoisikia sauti yangu, Sauti ilinena, "Simama, na ugeuke urudi nyuma."

53 Sasa nisingeweza kueleza haya miongoni mwa watu wasioamini. Yapasa ueleze haya kwa waaminio tu, na kisha, kwa sababu hii, wasioamini hawataelewa kamwe mambo haya. Yapasa uwe na nia ya kiroho ili uyaelewe mambo ya kiroho. Neno ni la kiroho. Latafsiriwa kiroho. Nalo—ni Neno la Mungu. Nami nilisimama, nikiwaza, "Kama nikirudi kule juu, nusu maili nyingine kule juu, na dhoruba inanguruma kwa namna hii . . .

54 Na David Wood alikuwa amenitengenezea sambusa, nayo, ilikuwa tamu sana! Nadhani alikuwa anaanza kusawazisha nami kwa kumtengenezea moja baba yake, wakati mmoja. Hatukuwa na kitu kingine ila vitunguu na asali na mkate, na, niliviweka vyote pamoja, tukajitengenezea sambusa. Na ilikuwa vigumu kwake kuila yake. Nami nadhani alikuwa anajaribu kusawazisha nami kwa ajili hiyo, hivyo aliweka . . . Sijui namna lile bonge . . . Na nilipokuwa nikipanda juu mlimani, mvua ilinyesha kasi, ikailowanisha, na ilikuwa ni bonge moja kubwa. Niliwaza, "Vema, nitakula hiyo na kungojea."

55 Na nilipokuwa nimesimama pale, niliwaza, "Hiyo haikuwa kitu. Nilidhania tu. Ulikuwa upepo, labda jinsi unavyopuliza, ukitikisa hii miti." Nami nilianza kutembea tena. Sikuweza kutembea. Nami niliwaza, "Vema, na—naamini nitarudi nyuma."

56 Nami nikaisikia tena, "Rudi ulikotoka." Ilisema hivyo. Nikaanza kupanda mlima, nikasimama. Nami nikawaza, "Huenda mimi . . . " Ni—nilianza kuogopa kurudi nyuma mahali nilikokuwa, kwa sababu ule—ule upepo ulikuwa wa kutisha mno.

57 Wakati mwingine Mungu hutufanya sisi tutende mambo ambayo—ambayo huonekana ni hatari sana na yaliyokwenda

kombo. Vipi kuhusu Musa na ile fimbo, akienda kuteka Misri? Na kila jambo tunalikuta namna hiyo, kwamba Mungu huwa anaagiza mambo yasiyowezekana, waona, hivyo kwamba Yeye hutenda mambo yasiyowezekana, ili kwamba mtu ajue kuwa siyo yeye mwenyewe; ni Mungu anayetenda jambo hilo.

58 Nilirudi tena kule juu ya kilele cha mlima, nikifuata njia kupitia katika miti iliyovuma, iliyokuwa inatikisika. Nami nikaketi chini na kuchukua bunduki yangu, na kuiweka darubini isipate. . . juu hivi, dubu hukimbia wakati kama huo, kwa hiyo niliweka darubini yangu tena ndani ya shati langu *hivi*, na kukaa chini kwa kitambo. Niliwaza, "Nafanya nini, kuketi hapa?"

59 Lakini Mungu hufanya mambo kwa mafumbo, kufanya maajabu Yake. Hayatambulikani, kwa akili ya kibinadamu. Hawapati kamwe tazamo la mara moja. Na niliporudi kule juu na kukaa chini, nilikaa nikiwaza juu ya Mungu. "Nashangaa kwa nini nimerudi hapa." Niliwaza, "Jamani, ni wakati wa kuteremka chini ya mlima, hiyo dhoruba inazidi kuwa mbaya sana wakati wo wote, ikifunika, hata huwezi kuona mbali mbele yako." Na sasa . . .

60 Na si lazima uamini hili, lakini hili ni kweli. Sauti ilizungumza na mimi, na kunena, "Mimi ni Bwana Mungu. Niliumba Mbingu na nchi. Maumbile yanitii."

61 Na ndipo nilikaa pale kitambo kidogo, nikavua kofia yangu upesi. Na hiyo Sauti, mahali fulani, sikuweza kuiona. Jambo pekee, niliweza kuisikia. Ilikuwa karibu katika ile miti, mahali fulani. Niliwaza. Kwa kawaida huona ile Nuru ambayo nyinyi nyote mnaijua, kwa kawaida huwa pale, lakini nilitazama kila mahali na sikuweza kuona ile Nuru. Nilisema, "Uko wapi Wewe, Ee Mungu, Muumba wangu?" Nilitazama huku na huko. Sikuweza kuisikia Hiyo tena, kuisikia Sauti Yake. Nikangoja kwa dakika chache.

62 Alinena, "Mimi ni Bwana Mungu ambaye alikuagiza wewe kunena hata kindi wakaumbika." Na nyinyi nyote mnafahamu jambo hilo. Na hivyo nisaidie, Biblia hii ikiwa mbele yangu, asubuhi hii ya Shukrani, kama hiyo si kweli, Mungu anaweza kuniulia humu jukwaani sasa. Waona, hii ni kweli. Yeye bado ni Muumbaji, Mungu—Mungu ambaye aliweza kumpa Ibrahimu kondoo, anaweza kutupa. Yeye bado ni Yehova-Yire. Bwana anaweza kutupa!

63 Ibrahimu alipata huyo kondoo wapi? Tazama, mwendo wa siku tatu mbali na ustaarabu, juu ya mlima, mahali ambako hakuna maji ama cho chote. Naye alihitaji kondoo na kulikuwa na kondoo amenaswa nyikani, kwa pembe zake. Na Ibrahimu alikuwa amezunguka na kuokota mawe, sehemu ile yote kutengeneza haya madhabahu; lakini Mungu bado alikuwa Yehova-Yire, Bwana atajipatia Mwenyewe.

64 Cho chote Yeye alichoahidi, hicho Yeye anaweza kutenda! Hilo ni Neno hilo katika Mathayo pale, nafikiri, ni Marko 11:22, “Ukiuambia mlima huu.” Mimi, mimi nilikuwa siwezi kuelewa hili. Mnajua kisa chake.

65 Na, hivyo nisaidie, hiyo ni kweli. Alinena, “Ni Mimi aliyekupa, hao kindi,” Yeye alinena. Sasa wakati . . . Nilisikiliza tena, kuona Yeye angesema nini. Hakuna kilichokoma; upepo ulivuma ukiendelea. La—lazima nijiume, kwa maana . . .

66 Hebu niwaambie jambo fulani. Nia ya kiroho halisi iko hatua moja kutoka kichaa. Je ulijua jambo hilo? Uchunguzi wa sayansi utakueleza hivyo. Hapa wewe uko chini *hapa* mzito na umefifia; na ndipo unakuwa wa kiroho zaidi, kisha unafikia kiwango *hiki*; kisha unakuwa kama shoka butu; na kisha unafikia kuwa wembe mkali. Sasa unajua upande gani ungeangukia hapo. Kama mtu akijaribu kujiinua mwenyewe juu hapo, kweli ataenda upande mbaya. Kama Mungu akimwinua juu pale, yuko juu sana kuliko mtu wa kawaida. Hapo ndipo maono na mengineyo yanatokea. Hapo ndipo Ufalme wa Mungu ulipo. Washairi, manabii, na wengine wote walihesabiwa kuwa wenye kichaa.

67 Yesu, Mwenyewe, aliitwa “mwenda wazimu.” Kasema, “Sisi tunajua Wewe una kichaa na una pepo.” *Kichaa* maana yake ni “mwenda wazimu.” Tazama washairi wote na manabii wote katika nyakati zote, walihesabiwa hivyo, ambao wanajaribu sana . . . kama wewe ukijaribu kujivuta hapo, umekwisha, kamwe hutafanikiwa. Inatakiwa Mkono ushuke kutoka katika Utukufu, kukushikilia kwenye mpaka ule, kati ya mambo mema na mabaya. Na unaposimama katika mipaka ile ndipo ambapo unatazama kule ng’ambo kwenye Nchi ya Raha.

68 Ndipo katika saa ile ile, ikanena tena, kwa wakati ule ule, nikiwa nimekaa juu kule. Akasema, “Mimi Ndimi niliyesimama kwenye mashua usiku ule, na kufanya upepo na mawimbi kukoma.” Kasema, “Simama kwa miguu yako na ukemee hii dhoruba, nayo itatii sawasawa na utakavyosema.” Hicho kimekuwa ndicho kile kiwango cha tatu cha huduma kikija. Ilikuwa ikiendelea kusogea, kwa miaka kadha. Na ilionekana kana kwamba kuna jambo linalonitia wasiwasi, ninawaza, “Loo, usifanye . . . ” Bali hilo ndilo hasa jambo Yeye alilofanya. Na huyu ni Yeye tena, ni Roho Wake tena hasa, kweli kabisa.

69 Lakini nimekuwa na maigizo ya kimwili mengi mno juu ya zile zingine, hunifanya ni hofu hata kuliwazia. Sababu mtakuwa na hilo, bila shaka. Siku zote kuna watu waliochangamana. Na hayo maigizo ya kimwili yatafuatisha Jambo hilo. Ilikuwa hivyo katika siku Zake, ilikuwa hivyo katika siku za Musa; itakuwa hivyo kila siku. Itakuwa hivyo katika siku hii wakati Roho Mtakatifu anajaribu kutenda zile kazi. Hata hivyo, kama mtu ni wa kiroho, maigizo ya kimwili yanakuza tu lililo kweli, Hilo, ki—kile kitu halisi cha Mungu.

70 Na nikiwa nimesimama pale, wakati huo, nilisimama na kusema, "Bwana Mungu, Muumbaji mkuu wa maumbile, naamini kwamba huyo ni Wewe unazungumza. Hakuna wakati hata mmoja ambao Wewe ulinionyesha jambo lolote ambalo ni kosa, na hakuna wakati hata mmoja ambao Wewe uliniacha niseme lolote isipokuwa tu lile ambalo lilitimia."

71 Nilisema, kwa hiyo, "Nasema kwa hii dhoruba inayonguruma, 'Nendeni makwenu. Rudini, ondokeni hapa. Tena naamuru kwamba jua liwake kwa siku nne zifuatazo, mpaka hawa watu waweze kupata wanyama wao, nami nipate kuwasaidia kuwapata, na kutoka katika hii milima.'"

72 Na Bwana Mungu, Ambaye ndiye hakimu wangu mwaminifu asubuhi ya leo; hiyo mvua na kadhalika vikipindika, katika kufumba na kufumbua havikuwapo hata kidogo. Nilitazama na kulikuwa na upepo uliotoka upande ule mwingine, kupitia kilele cha mlima, na kuyachukua yale mawingu hivyo. Katika muda wa dakika chache tu, jua likatokeza, kupitia kile kilele, likiangaza kule chini, vizuri iwezekanavyo.

73 Kama vile ilivyotokea Ujerumani. Mnakumbuka kisa cha Ujerumani. Wakati, wale wachawi, kumi na watano wakiwa upande mmoja, walikata, walichukua makasi na kukata unyoya, wakauelekeza nyuma hivi, na kusimama pale wakinuiza uchawi wao, kisha wakasema wangelipua lile hema, la watu elfu thelathini. Na Ndugu Arganbright alikuwa amesimama pale. Na hapa ikaja dhoruba, wingu likaja moja kwa moja. Nilisimama pale karibu na Ndugu Lowster. Wengi wenu mnamfahamu, Mjerumani mzaliwa wa Amerika hapa ambaye ni mkalimani wangu kule. Na yeye—yeye alisimama mahali pale. Nilisema, "Usitafsiri hili." Lakini nilisema, "Bwana Mungu, Wewe ulinipa o—ono na kunituma Ujerumani. Hawa wachawi wameleta dhoruba. Wewe ni Mungu wa uumbaji, hebu na ijulikane kuwa Wewe ni Mungu!" Hakuna mtu ila yule aliyeelewa Kiingereza, na hao hawakufika watu dazani moja walioweza kuelewa niliyokuwa nikisema.

74 Papo hapo lile hema likiinuka juu *hivi*, likiwa na watu elfu thelathini chini yake, liliruka-ruka juu na chini *hivi*, mara lilitulia, na mawingu na ngurumo vikaondoka. Katika muda usiotimia dakika tano, jua lilikuwa liking'aa chini, wakati Wajerumani wapatao elfu kumi na tano walimjia Bwana Yesu Kristo. Yeye bado ni Mungu. Yeye yu Mungu vivyo hivyo kama vile amekuwa wakati wote.

75 Naam, niliposimama kule juu ya mlima. Nikitoka baada ya siku nne, ye yote hapa anajua ukweli, hapakuwa na wingu hata moja katika anga, kutoka saa ile, kwa muda wa siku nne.

76 Nilipoteremka na kuondoka, kwenda, kununua petroli tukisha kutoka milimani, nilisema, "Hatukupata unyevu wowote."

77 Kasema, “Naam, hamna unyevu.” Kasema, yeye akasema, “Tulikuwa tunatazamia dhoruba hivi majuzi, ikaja, lakini hatujui, kitu hicho kikakoma.” Waona?

78 Nikashuka nikaenda upande wa pili wa Colorado, nikasimama kununua petroli. Billy, Paul, mwanangu kule nyuma, tulikuwa pamoja. Nikasema, “Hebu tuone kama ilikoma huku chini.”

79 Nami niliingia na gari, nikasema, “Habari za asubuhi,” na hivyo tulianza kuzungumza na yule mtu.

Akasema, “Njema.” Naye . . .

Nikasema, “Hakika ni siku njema!”

80 Akasema, “Ndiyo, jua la kale limechomoza kali tena.” Alisema, “Hakika limetuchoma katika kiangazi hiki.”

81 Nami nilisema, “Ndiyo.” Nilisema, “Naam, hiyo ni kote nchini.”

Akasema, “Ndiyo, naelewa.”

Nami nilisema, “Wakati wa dhoruba zenu umekaribia,”

82 Akasema, “Je, wajua?” Akasema, “Magazeti yote, redio, na kadhalika, yalitangaza kuwa dhoruba ingekuja hivi majuzi. Na ndipo mawingu yalikusanyika, na dhoruba ikaanza. Mara, hatujui nini kiliipata, yote ikatoweka.”

83 Yeye bado ni Mungu, ni Mungu hasa kama alivyopata kuwa. Lakini mtu awezaje kusema mambo hayo isipokuwa Mungu amemwambia kwanza aseme hayo? Waona, siyo dhana; bali unajua jambo unalosema, ndipo unafanya hivyo. Lakini ngoja, usijaribu kusema, “Loo, hiyo ndiyo njia!” Watu wengi nadhani, na—na karama za Mungu . . . Ngojea ujue ndivyo ilivyo, ujue ni Mungu. Waona, ngoja mpaka Sauti ije, na uisikie, na uijue, uione, ndipo unaweza kusema, “Ni BWANA ASEMA HIVI.” Kama siyo BWANA ASEMA HIVI, ndipo inakuwa ni dhana yako, ni vile mtu mwingine anavyodhani. Watu huwaomba watu, “Sema *hili* kwa ajili yangu. Tenda *hili* kwa ajili yangu.” Unawezaje kutenda hayo, kama wewe ni mwaminifu kwa Mungu, hadi Mungu akwambie kwanza? Nawezaje kukwambia, “Jack Moore asema hivi,” na Jack Moore hajasema lolote kwangu? Unaona? Lazima kwanza litoke kwa Mungu, siyo kudhania. Lazima awe ni Mungu, na ndipo litatokea, kwa maana basi ni BWANA ASEMA HIVI.

84 Sasa, kila mtu hatakuwa na jambo hilo. Hapana, bwana. Haitakuwa hivyo. Kamwe haikuwa hivyo. Kamwe haitakuwa hivyo. Mungu hushughulika na mtu binafsi. Yeye alifanya hivyo katika siku za Nuhu. Alifanya hivyo katika siku za—za Yoshua. Alifanya hivyo katika siku za Musa. Siku zote amefanya hivyo. Yeye hajawahi kuunda chama. Imekuwa ni mtu mmoja binafsi, kwa sababu watu wawili hawalingani, hata wakati mmoja. Waona, kamwe Yeye hakuwahi kufanya hivyo. Lakini kila mtu

haikumpasa awe Musa. Wao hawakuelewa hilo; walifuata tu. Na Roho Mtakatifu, kama mtu ana upako wa Mungu, atakuongoza umfuate Roho Mtakatifu na Biblia, kwa maana Yeye Ndiye anayefanya mambo haya, Yesu Kristo katika umbo la Roho Mtakatifu akitenda kazi katika watu.

85 Nikisimama pale, nilianza kurudi nyuma. Nilisimama pale. Nikalia. Sikuweza kujizuia, nikiona mambo yaliyokuwa yametokea pale katika muda mfupi.

86 Na ndugu waliokuwa kule, sasa ni wangapi walikuwako, kuna mtu hapa? Najua Fred Sothmann na wengineo wako hapa, waliokuwa juu kule; hapana, Fred alikuwa pamoja nami mahali pengine. Yupo yeyote hapa sasa ambaye alikuwako juu kule? Je Ndugu Banks Wood na wengine wamefika? Kuna mtu yeyote hapa mbali na Billy Paul ambaye alikuwako juu kule? Hawa wavulana walikuwa tu wameondoka, ndiyo, na Ndugu Wood, na Ndugu Taylor, au, nimesahau jina la ndugu yule mwingine, wanne ama watano wao walikuwa wamesimama pale. Hawa ndugu hapa, Ndugu Martin alikuwa tu ameondoka, aliondoka siku moja mbele, kwa ajili ya dhoruba iliyokuwa inakuja. Nyote mnaikumbuka ile dhoruba, matangazo, walisema kwamba ilikuwa inakuja. [Ndugu mmoja anasema, "Tulikutana nayo."—Mh.] Sasa, umesemaje? Mlikutana nayo. ["Tulikutana nayo."] Mlikutana nayo.

87 Kisha, na sasa angalia. Nilisimama pale, niliwaza, "Naam, nadhani nitatelemka chini ya kile kilima."

88 Nami ni—niliweka nadhiri kwa Mungu, miaka michache iliyopita, nilipokuwa naambatana na Wafanyi Biashara wa Injili Yote, kwamba, "Nisingepiga mnyama risasi kwa ajili ya mtu mwingine, isipokuwa ni kwa dharura." Nisingefanya hivyo.

89 Na, ndiyo, ilikuwa ni Ndugu Jack Palmer, je yuko hapa? Ndugu Jack, alitoka Georgia, kwa kawaida huwa anakuja hapa. Alikuwa amesimama pale. Na usiku mmoja hapo mbeleni, alisema, "Ndugu Branham, niwindie kulungu mmoja."

90 Na, jamani, nilitetemeka, kwa sababu, na—najua niliweka nadhiri kwamba nisingefanya jambo hilo, miaka minne au mitano iliyopita, sababu mwaka huo niliua kulungu wenye pembe pandapanda kumi na tisa, peke yangu. Kwa ajili ya wafanya biashara ambao hukaa kitako kuzungumzia biashara zao. Ingenibidi kwenda na kuua wanyama kwa ajili yao. Na jambo hilo halikuonekana. . . ni kama kuniweka katika fungu la wauaji, lakini nisingefanya hivyo. Nitawapeleka kule waliko, lakini sitawapiga risasi. Kwa hiyo nilimwahidi Mungu kwamba nisingefanya jambo hilo.

91 Hivyo basi, nilikuwa, nimeondoka mahali pale, nikirudi nikaanza kuteremka kilima, na Sauti ilizungumza nami, na kusema, "Kwa nini usitembee pamoja Nami?"

92 Nami nilisema, “Bwana Mungu, ikiwa huyo ni Wewe, najua kwamba ni mkono wa Mungu pekee unaoweza kuyatawanya yale mawingu na kutenda yale Wewe umetenda hapa.” Na jua lenye joto linawaka, linakausha shati langu, na mvuke unatoka ndani yake. Nami nilisema. . .Hekalu kuu, msitu usioguswa, unajua. Nami nilisema, “Naamini nitatembea kuelekea upande huu basi, Bwana, kama Wewe huna upande maalum. Nilitaka kwenda juu kule na kusimama kwa dakika chache kwa ajili ya kumbukumbu ya mke wangu, ya—ya fungate yetu ya kwanza na ya pekee, unajua, ambayo tuliwahi kupata nafasi kuifanya. Nami nilimpeleka katika ziara ya kuwinda, na sasa niko hapa tena mwaka huu, nikiwinda pamoja na hawa ndugu; naye yuko kule chini Tucson, akijaribu kuyaendeleza mambo.”

93 Nami nilianza kutembea kupitia pale, na nilianza kuwaza. Sasa hili litaonekana kama mzaha. Nami nitaharakisha, kwa sababu najua ibada yenu itaanza katika dakika kumi zijazo. Na hivyo nilikuwa natembea kupitia chini pale, nami nilikuwa nikiwaza, “Loo, nashangaa kwa nini hakuwahi kuniambia neno kuhusu kwenda popote?” Na asubuhi ya leo nataka kuwaeleza yaliyotokea, kwa dakika chache. Mimi—mimi . . .

94 Kila mwanaume anapaswa kufikiria hili. Na—nafikiri hakuna mwanamke duniani kama mke wangu. Ni mtu mzuri sana, mtawa, anayekaa nyumbani. Sikuzote amezitayarisha nguo zangu. Na ninapokuwa nje, niko safarini, kila kitu; nakuja, nasema, namtania kidogo, nasema, “Mimi ni mume wako. Je wewe ni mke wangu?” Na mambo kama hayo, na nawabusu watoto, napiga magoti na kuomba; na navaa nguo zangu nisije nikarukwa na akili, ingaliwezekana, kwa ajili ya msongamano wa makutano na mambo mengine, nashika njia kwenda kuvua samaki au kuwinda, mbali naye. Amelazimika kuvumilia yote hayo peke yake, mwenyewe.

95 Kisha nilianza kuwaza, “Naam, huenda ikawa wakati ninapokuwa nyumbani, jambo pekee mimi sikuzote. . .jambo pekee ninalojua ni Mungu na Neno Lake. Nami daima nazungumza kuhusu Hilo.” Na nilikuwa nikiendelea pale, na wazo fulani likanijia, kasema, “Vema, huenda ikawa alikuacha uende kwa sababu ina—inawafanya watu wasije, na mengineyo kama hayo. Naye anaweza kidogo akawa na amani zaidi usipokuwepo.” Nami nilianza kulifurahia hilo wazo. Nilifanya, “Um,” hivyo, na, wakati nilipofanya hivyo, niliona sharafa katika uso wangu, za muda wa juma moja, na zaidi ya nusu zilikuwa mvi. Niliwaza, “Bill, umekuwa . . . unajua unakoelekea. Wewe unaelekea kwisha sasa, waona, unakuwa mzee. Na umekwisha vuka umri wa miaka hamsini.” Basi nilikuwa tu nikiwaza hayo, nikiendelea na bunduki yangu ikining’inia kwenye bega langu, nikiendelea kutembea namna hiyo.

96 Na kwa ghafla, jambo fulani likatokea. Ilionekana kana kwamba, kwa kila namna, nilikuwa mvulana tena. Sijui

ilitokea nini katika akili yangu, au ilikuwa kitu gani. Nami nilitazama, nikisimama mbele yake, na hapo mbele yangu, naye alisimama pale amekuwa kama vile alivyokuwa wakati nilipomuoa. Niliweka bunduki yangu chini. Nikapangusa macho yangu. Nikamtazama naye akanyosha mikono yake namna hii, akanitazama. Nikainamisha kichwa changu chini.

97 Maana, nilikuwa nakwenda pale kwa ajili ya kumbukumbu ndogo ya—ndogo ya sikukuu ya ndoa yetu; kusimama karibu na ile miti, chaka la miti midogo juu kule, waliko vifutu watetemekao, kama waliokuwa katika vichaka vya kaskazini wakati tulipokwenda Adirondack. Nami sikuzote huenda kule, kila tarehe ishirini na tatu Oktoba, wakati ninapokuwa kule.

98 Naye alikuwa pale. Nami niliweka bunduki yangu chini, nikatazama pale. Nami nilitulia kwa dakika moja, kisha nikainamisha kichwa changu. Nikatazama tena, naye alikuwa bado amesimama pale amenyosha mikono yake. Nami niliwaza, "Hakika sijarukwa na akili." Nilitazama tena. Nikawaza, "Kwa nini imekuwa hivi?" Nilikuwa hapa, kijana mdogo. Nikaitazama mikono yangu, nikasema mimi . . . "Bwana, wajibu wangu ulimwenguni, kuuleta Ujumbe Wako, hakika kuna jambo limenipata." Nami nilitazama tena, na ndipo ikatoweka.

99 Nami nilichukua bunduki yangu, nikaiweka begani mwangu. Nami nilisema, "Huenda ikawa huyo ni Wewe unanijulisha sababu yake, anavunjika moyo inaponilazimu . . . ninapoingia, na kutoka kwenda kuwinda, na mambo kama hayo."

100 Lakini nilipoanza kutembea, nilivua kofia yangu tena. Nikasema, "Mungu, najua kwamba wewe uko hapa. Hamna shaka niani mwangu kwamba Wewe uko hapa. Nami nakuamini Wewe, kila Neno. Wewe, Wewe unalifanya lile jua liangazie kwenye mgongo wangu. Wewe Ndiwe unayefanya mambo haya. Wewe ni Muumbaji. Mimi, nimekuwa mvivu sana, yaonekana kana kwamba naogopa kushikilia. Naogopa nitafanya kosa." Nikasema, "Kuna jambo moja nitakuomba Wewe ufanye. Niondolee mzigo huo moyoni mwangu. Hakuna haja kwangu mimi kujaribu kukiri tena, kwa sababu kwa miaka mitano nimeendelea kukulilia Wewe. Nimefanya nini? Niambie ni kitu gani."

101 Nami nilikuwa napanda kile kilima kidogo wakati huo, karibu na mahali nilipokuwa nakwenda kusimama kwa dakika chache, kumshukuru tu Bwana kwa ajili ya mke wangu na ndoa yenye mafanikio ambayo Mungu alitupa, na upendo tuliokuwa nao, miaka hii, na watoto wetu. Nami nafanya hivyo kila tarehe ishirini na tatu Oktoba. Na hapo alikuwapo kifufu mdogo atetemekaye, anakaribia, loo, inchi kumi urefu, alikuja karibu *hivi* na akaondoka, kwa mfano wa L, na akaenda zake juu.

Na nilikuwa napanda kilima, nilijisikia mdhaifu kabisa, na nikauegemea ule mti, *hivyo*.

102 Nami niliweza kusikia kitu kikipigapiga kwenye majani, kwa dakika moja tu. Sasa, majani yalikuwa yamekauka mnamo wakati nilipofika pale, yapata yadi mia tatu au mia nne. Nami nilitazama, na kumbe ilikuwa ni machozi yakitoka katika macho yangu mwenyewe, yakitiririka, kupitia katika ndevu zenye mvi, kwenda chini ardhini. Nilisema, "Ee Mungu, mimi ni—ni mtu aliyeshindwa kabisa." Na nikisimama pale katika hali hiyo. Nikasema, "Mimi—mimi nasadiki kwamba Wewe utamrehemu." Nikasema, "Mimi—mimi sistahili kuomba rehema." Nikasema, "Siku moja, najua nitakuwa na mvi, na si—sina budi kuondoka, Bwana."

103 Nami nadhani watu wanafikiri mimi ni wazimu, bali mimi—mimi humwona Mungu katika sehemu hizo. Hapo ndipo—hapo ndipo panakuwa mahali halisi kwangu. Mimi . . . Ni—ni halisi kama ilivyo hapa; na kwa kweli, ni zaidi kidogo, sababu, waona, nyinyi nyote, ni sehemu. Kule, inaonekana kana kwamba nasimama na Yeye peke yangu, nikizungumza na Yeye peke Yake.

104 Na niliposimama pale, nilisikia vijiti vikivunjika-vunjika, nami nikainua kichwa changu juu; nikiwa na shati nyekundu sasa, na ukanda mwekundu kuzunguka ko—kofia yangu, kitambaa chekundu kimekunjwa kuzunguka moja ya hizo kofia za kimagharibi. Nami—nami nilitazama, na hapa walisimama wawili, kulungu watatu wakisimama karibu nami; walitembea mpaka hapo; mimi nikiwa nimevaa hiyo nyekundu. Kupiga bunduki kote kule, watu mia moja, walikuwa wamerushiwa risasi mara arobaini, nadhani; naam, hakika, wangekuwa wametawanyika sasa hivi. Lakini hawakufanya hivyo. Walisimama tu na kunitazama mimi.

105 Na wenye nyama nzuri, watoto wawili wa kulungu waliokomaa na jike mmoja. Na kitu fulani kiliniambia, "Huyo hapo kulungu kwa ajili ya Ndugu Evans, na mmoja kwa Ndugu Welsh, na mmoja kwa ajili ya mhubiri Mmethodisti. Hao hasa ni Bwana Mungu amekupa wewe sasa. Hawawezi kukimbia. Hawana njia ya kufanya hivyo." Nilikuwa na bunduki ikining'inia kwenye bega langu papa hapa. Na hata kabla hawajageuka, ningekuwa nimewaua wote watatu, waona, namna hiyo, kabla hata hawajasogea. Walikuwa mkononi mwangu kabisa. Nami . . . Nami—nami nikawaza, "Wako hapo, hao watatu. Ni rahisi kuwafingirisha chini ya kilima hapa, na kisha kuwabeba kuondoka nao." Nami niliwaza, "Hiyo ingekuwa rahisi. Hapo wako watatu, kisha tungekwenda nyumbani basi, kuwachukua na kuondoka milimani." Na nilipowaangalia pale, walikuwa wamesimama, wakinitazama, kimya kabisa, yapata yadi kumi na tano, ishirini hivi. Vema, nilisimama kimya.

106 Na sijui kama nyinyi jamaa huwinda kulungu, au hapana, lakini wanachekesha, wakati wao—wao hawana . . . au hawana hakika, wataweka miguu yao *hivi*, waende . . . [Ndugu Branham anachapua miguu yake taratibu, kisha anaibadilisha—Mh.]

107 Halafu wakaniangalia mimi. Nikawaza, "Naam, wako hapo. Jambo pekee, ni kuwafyatulia bunduki yangu nao wame—wamekwisha."

108 Na ndipo nikakumbuka nilimuahidi Mungu kwamba nisingetenda jambo hilo. Nami nikakumbuka hilo. Niliwaza, "Hapana, sitatenda jambo hilo. Hiyo si haki. Nilimuahidi Mungu kwamba sitafanya hivyo." Na wakati unapotoa ahadi, itimize. Mungu anakutarajia kufanya hivyo. Na hapa nikawaza, "Vema, wako mikononi mwangu kabisa, hata hivyo nilimuahidi Yeye nisingetenda jambo hilo."

109 Nilisema, "Nenda, mama, chukua watoto wako na uende kichakani, jifurahishe mwenyewe. Napenda jambo hili, pia. Mko mikononi mwangu, lakini sitawaua." Na wakasogea karibu zaidi. Loo, siyo jambo la kawaida, kwa kulungu. Nao wangenitazama mimi, unajua, na kisha wakageuza vichwa vyao. Na mimi nikisimama pale, nimevalia mavazi mekundu, na bunduki iko mkononi mwangu. Nao walisogea karibu kabisa hata karibu wangeweza . . . ningeweza kuwalisha kwa mkono wangu. Nao walinusa-nusa kila mahali pale, kitambo kidogo, wakageuka, wakarudi nyuma kidogo. Wakasimama, wakaja tena.

110 Kitu fulani kiliendelea kusema, "Wako mikononi mwako kabisa. Wako mikononi mwako kabisa. Bwana amewaweka mikononi mwako."

Nikasema, "Lakini niliahidi, niliahidi kwamba sitatenda jambo hilo."

111 Tangu hapo, nikawaza, "Unajua wakati mmoja, Daudi aliongozwa mpaka mahali hasa Yoabu alikuwa amelala na . . . au mahali Mfalme Sauli alikuwa amelala. Na Yoabu akamwambia, akasema, 'Bwana amemtia huyu mikononi mwako.' Bali yeye alisema, 'Hasha, sitamgusa mtiwa mafuta wa Mungu." Unaona? Waona, lazima uwe mwangalifu wakati unapotoa ahadi.

112 Na kisha nikasema, "Nilimuahidi Mungu kwamba nisingetenda jambo hilo, kwa hiyo sitalitenda."

113 Nikasema, "Mama, chukua watoto wako uende huko vichakani. Sitawasumbua. Mko mikononi mwangu, msingeweza kutoroka hata mkifanya nini. Lakini mimi—mimi sitawadhuru. Nendeni zenu vichakani." Nao wakarudi tena, wakanizungukia kabisa. Na mimi nilisimama pale. Nami nikawaza, "Ni jambo gani hili? Jambo la kushangaza."

114 Mimi ni mtu anayependa maumbile. Mimi—mimi—mimi namwona Mungu katika maumbile, kutua kwa jua na

kuchomoza; ni kifo, ni uhai, ma—mazishi; kufa, kufufuka tena, mambo yote. Kama vile miti, jinsi Ayubu alivyosema kuhusu kujificha katika kaburi, "Yeye ataniweka katika patakatifu." Tena angalia utomvu ukiondoka kwenye miti, na kwenda chini katika kaburi la mizizi, na kurudi tena katika majira ya kuchanua, ufufuo. Kila kitu kinazungumza juu ya uhai na ufufuo.

115 Na nilipokuwa nimesimama pale nikiwaangalia, walisogea karibu zaidi, karibu zaidi. Kisha wakageuka na kutembea vichakani. Nami nikasimama pale kama tu kwamba nimeshikwa na bumbuazi.

116 Na wakati walipoondoka, ile Sauti ikazungumza tena, huku lile jua linawaka mgongoni mwangu, ikasema, "Uliikumbuka ahadi yako, sivyo?"

117 Nilisema, "Ndiyo, Bwana, niliikumbuka ahadi yangu. Najua huyo ni Wewe. Siwezi kukuona Wewe, Bwana, lakini Wewe uko hapa mahali fulani." Nikasema, "Sikuoni Wewe, lakini nasikia Sauti Yako. Najua Wewe uko hapa."

118 Kasema, "Ulitimiza ahadi yako, umekumbuka ahadi ya—yako. Mimi nitakumbuka Yangu, pia. Kamwe sitakupungukia wala sitakuacha."

119 Loo, jamani, sijajisikia vile tena tangu wakati huo! Niliteremka mlima. Adhuhuri yote, ono baada ya ono likatokea, likitendeka. Niliteremka. Yaonekana kana kwamba kila kitu kimebadilika tangu wakati huo. M—mzigo umeondoka.

120 Kuhusu wakati huduma iliponijia kwanza, kwa kuhisi kwenye—kwenye mikono ya mtu, jambo ni kwamba, ilikuwa uhai uliokuwa ndani yao, na—na tunajua jinsi ilivyoenda.

121 Usiku mmoja, kule California, nilikuwa nimekaa na familia ya Malicki, Ndugu Moore anakumbuka na Ndugu Brown, familia ya Malicki. Na huyo bibi mdogo alikuwa apatwe na ugonjwa wa kuvilia mguu, tangu alipozaliwa. Na mimi—mimi nilimfanya anyoshe mkono wake, nikasema, "Uko hapa, unaona kutetemeka kwake. Unaona?" Nami nilisema, "Wewe, utavilia miguu." Nilisema, "Tayari inatenda kazi ndani yako." Na aliugua, karibu apoteze maisha yake.

122 Na Ndugu Malicki aliniuliza, akasema, "Ndugu Branham, jinsi gani unatenda haya?"

Nilisema, "Sijui. Siwezi kukueleza jinsi yanatendeka. Ni Mungu."

123 Na hivyo niliinua mkono wangu namna *hii*. Nikasema, "Hapa, huyu hapa mke wangu, najua hana kasoro yo yote. Laza mkono wako juu ya mkono wangu, mpenzi." Naye alifanya hivyo, na hapo uvimbe ulitetemeka, kutoka matezi ya kike. Nami nikasema, "Mpenzi, una uvimbe, mpenzi, katika matezi ya kike."

Naye akasema, "Si—sisikii kitu."

124 Nikasema, "Mpenzi, huu hapa kwenye mkono wangu. Inua mkono wako juu." Aliinua, kisha kauweka chini tena. "Unaona?"

125 Naam, wakati tulipoondoka, tukaja nyumbani, tunaye daktari mzuri sana; tulisoma shule pamoja. Tulimpeleka kule, kwa uchunguzi. Alisema, "Billy, hakuna kasoro yo yote kwake." Akasema, "Ni mzima. Hakuna uvimbe hapo."

126 Nilisema, "Sam, sipendi kutilia shaka neno lako, waona, kwa sababu umemfanyia uchunguzi, lakini kuna uvimbe hapo."

127 Kila mtu, zaidi ya miaka mitatu au minne, wakati ninapokwenda kufanyiwa uchunguzi wa mwili, wakati ninaposafiri nchi za ng'ambo, mke wangu hufuatana na mimi kwa uchunguzi wa mwili. Na wakati wanapofanya hivyo, hawajapata kuuona.

128 Na yapata miaka miwili iliyopita, nilikuja nyumbani siku moja, sasa mimi—mimi lazima niwaeleze ukweli wote. Mwaona, hupendi kuacha jambo lo lote, lazima ueleze ukweli wote. Nami nimewaeleza, upendo wangu kwa mke wangu. Hata hivyo yapasa tuwe waangalifu katika mambo hayo. Ninawaambia ukweli. Baba wa Mbinguni, ambaye ni Shahidi wangu hapa tulipo sasa, anajua ni kweli. Loo, pale nyumbani, jinsi palivyo, *hili, lile,* na mengine yote! Maskini mke wangu anapitia katika mabadiliko ya maisha wakati huu, anapoacha kuwa na hedhi.

129 Na kwa miaka michache iliyopita, yapata miaka miwili iliyopita, wakati nilipofanyiwa uchunguzi, ndipo daktari aliona uvimbe juu ya mfuko wa mayai ya uzazi upande wa kushoto. Ulikuwa umekua kufikia ukubwa wa—wa jozi. Alisema, "Hebu niufanyie huo uchunguzi tena, Ndugu Branham." Akasema, "Kufikia miezi mitatu, kama utaendelea kukua, lazima utokee." Naam, kisha sisi . . .

130 Lakini kabla tu ya hilo, nina jambo fulani la kuwaambia. Nilisahau jambo hilo. Siku moja nilikuja, na kutoka nyumbani, na nilikuwa nimekuja kufanya jambo fulani, na kisha niligeuka na kutoka. Nami nilisema . . . Alisema, "Je unaweza kwenda mjini pamoja nami, Bill?"

Nami nilisema, "Siyo sasa hivi, mpenzi."

131 Naye akasema, "Je tutafanya nini kuhusu Becky, juu ya jambo *fulani*?"

Nikasema, "Naam, mpenzi, sijui tutafanya nini."

132 Na hapo jambo fulani likatokea, na yeye akaingiwa na fadhaa mno hata hangeweza kujizuia. Watu nyumbani, usiku kucha. Na kama ilivyokuwa usiku wa kuamkia jana, hadi saa saba ya usiku, watu walikuwa wanakuja, kuzunguka nyumba, kuzunguka madirisha na kila . . . Hivyo basi akafadhaika sana, naye akaniambia jambo fulani, kwa hamaki, ambalo hakupaswa

kulisema. Unaona? Alisema, “Basi, Bill, sikuzote unasafiri, nami yanibidi kuwalea hawa watoto peke yangu.” Akasema, “Sikuzote hupatikani hapa. Hatuwezi kufanya maamuzi yetu pamoja. Mara umetoka, umesafiri,” naye akaanza kulia, akaingia ndani na kufunga mlango.

133 Papo hapo nikasema, “Loo, maskini mwenzangu!” Nikasema, “Jamani, yanipasa . . . ” Nami nikaanza kutoka nje.

134 Kisha Hiyo ikasema, “Soma II Mambo ya Nyakati 22.” Ilikuwa wakati Miriamu alimkemea Musa, kwa kumwoa msichana Mkushi; ingekuwa heri kama baba yake angemtemea mate usoni, kuliko kufanya jambo hili.

135 Nami—nami nikaingia ndani, nikasema, “Mpenzi, umesema jambo baya.” Naye alikuwa akilia. Nikasema, “Umesema jambo baya, mpenzi. Mungu atakulipiza jambo hilo. Hukupaswa kufanya hivyo. Nimechanganyikiwa mimi mwenyewe. Hukupaswa kusema jambo hilo.”

136 Naye akasema, “Naam, Bill, mimi—mimi nimechanganyikiwa mno.” Nami niligeuka nikarudi maana nilijua kuwa hakuwa katika hali ya kulipokea hilo, hivyo nilitoka nje.

137 Na uchunguzi uliofuata, yapata muda wa mwezi mmoja baada ya tukio hilo, ulionyesha ule uvimbe.

138 Mwaka uliopita ukaonekana tena. Wakati alipojaribu tena, sasa ulikuwa mkubwa kama chungwa. Daktari akasema, “Usimcheleweshe zaidi. Lazima afanyiwe upasuaji. Huu ni uvimbe unaokua haraka sana, unaua. Kama ukienea kila mahali, na kusonga ubavuni, mtafanya nini?”

Nikasema, “Daktari, tunamwamini Mungu.”

139 Sikuliambia kanisa, au ye yote yule, niliacha iwe hivyo. Tulianza kuomba. Nami nikasema, “Bwana Mungu, tusaidie, tafadhali. Naomba kwamba utatusaidia,” na kuendelea namna hiyo. Uvimbe huo uliendelea kukua zaidi na zaidi.

140 Kisha wakati tulipoondoka kwenda Tucson, daktari wetu kule nyumbani alituma habari kwa daktari rafiki yake aliyeko kule, kasema, “Ni lazima uondoe huo uvimbe ndani ya Bi. Branham, mara moja.” Akasema, “Kama hutafanya hivyo, huo utasababisha kifo.” Akamueleza, akisema, “Huo uvimbe tayari umekwisha kua, katika mwaka mmoja, kutoka ukubwa wa jozi hadi ukubwa wa balungi,” ulikuwa mkubwa sana. Ulikuwa hapo, umesonga ubavuni mwake, namna *hiyo*. Na hivi majuzi . . .

141 Yeye—yeye alikuwa ameacha, kwenda; nilisema, “Jaribu . . . ” Tuliomba. Tulilia. Tulisihi, kila njia, hakuna kitu kilichotukia. Ndipo alikuwa anakwenda, mwishowe ilimlazimu kwenda . . . hebu tuone, jana. Ndiyo, jana alikwenda kwa daktari kwa mara ya mwisho. Nilisema, “Naam, nachukia kufanya jambo hilo,

lakini huenda itatubidi kukubaliana naye. Na ndipo, mpenzi, u—utapaswa ku—kukubaliana naye, kuacha . . . kuacha utolewe, maana unazidi kuwa mkubwa sana, imani yetu haitoshi."

142 Kwa hiyo, juzi, kabla sijaondoka, akijua, alisema, "Usinipigie simu mpaka baada ya ibada ya Ndugu Jack usiku huo, ndipo unieleze mlikuwa na mkutano wa namna gani, na watu wana hali gani huko Shreveport. Kisha," akasema, "nitakueleza yale daktari alisema."

Nilisema, "Sawa, mpenzi." Nami nikaiweka chini.

143 Jana, juzi, wakati nilipoanza kuondoka pale, nyumbani, nilikwenda ndani na . . . Sikuzote wakati tunapoondoka, watoto sote na sisi wote kwa jumla tunakusanyika pamoja na kupiga magoti pale chumbani, na kuomba. Na Bwana, tunamwambia Bwana . . . Ninaposafiri nchi za ng'ambo, nasema, "Bwana Yesu, ilinde familia yangu." Nao wananiombea mimi, ili Mungu anisaidie, tuweze kukutana tena. Kisha watoto wote wanaanza kulia na kadhalika, mnajua, maana, mnajua mambo hayo yalivyo.

144 Nena kuhusu Rais Kennedy kupigwa risasi? Imenibidi kulindwa mara nyingi nisipigwe risasi kwa bunduki ya darubini, na labda kwa umbali wa yadi mia tatu au mia nne, usiku. Wanaweza kuona sawasawa tu na vile wanavyoona wakati wa mchana, kwa kutumia hiyo darubini ya shabaha usiku. Nami nimekuwa katika nchi za Wakatoliki mahali ambako watu wenye msimamo mkali wa kidini na wengine wote, kule Mexico mahali ambako walitumana pale, na walituma habari, jumbe za simu zimeandikwa kila kitu, "Tutakupata usiku wa leo," na mengine kama hayo, wakiingia na kutoka, wakinitafuta mimi. Na labda nitaipata wakati fulani. Hiyo ni sawa. Lakini ninacho Kitu kitakachonilinda wakati huo utakapofikia, waona.

145 Na ndipo wakati nilipoanza kuondoka tena, peke yangu, hivi majuzi, nilipiga magoti, juzi, na nilipiga magoti ndani ya chumba. Na nikatazama huku na huko. Nilikuwa pale kwa siku kadha, katika upweke, hapakuwa na mtu mwingine pale nyumbani. Nami nikasema, "Baba wa Mbinguni, na—naomba kwamba Wewe utanirehemu sasa, na unisaidie mimi. Nakwenda kule Shreveport kufanya kila niwezacho kuusaidia Ufalme Wako." Nikasema, "Mara ngapi mimi na mke wangu tumepiga magoti hapa ndani ya chumba namna hii! Tukaomba. Na leo nasikia upweke mno kwa ajili yake." Nami nikasema, "Kesho atakwenda, na labda sitaweza kumaliza mikutano yangu, kwa sababu huenda ikawa atapelekwa hospitalini, kwa ajili ya uvimbe huu mkubwa ambao tumekuomba Wewe umuondolee. Umeendelea sana kukua, hadi sasa yapasa uondolewe." Nami nikasema, "Mimi—mimi nimekusihi Wewe sana."

146 Nami nikasema, "Bwana, kama alikosea katika kusema jambo lolote, wakati yeye . . . wakati ule, nilipochanganyikiwa.

Kama yeye alikosea kusema jambo lolote," nikasema, "Bwana, kumbuka, yeye hajawahi hata mara moja, hata mara moja hajawahi kusema lolote kwangu kuhusu kwenda katika mikutano Yako." Nikasema, "Wewe uta . . . Yeye sikuzote amefua nguo zangu na kuziweka tayari, na kunishika mkono, na kulia na kuomba, na kusema, 'Kama ningeweza kufanya jambo lo lote la msaada kwa Bwana!" Nami nikasema, "Iangalie hali yake, Bwana. Na usi—usifanye hivyo. Usifanye hivyo, tafadhali usifanye hivyo, Bwana." Na—nami nikasema, "Mungu, msaidie, naomba kwamba Wewe utamrehemu. Na kama itambidi kufanyiwa upasuaji, msaidie hata mwisho, Bwana. Kama ningempoteza sasa, sijui ningefanya nini. Mimi—mimi ni mzee. Na watoto hawa wachanga kupata malezi, ningefanya nini? Umrehemu, Bwana. Wewe unajua jinsi ninavyompenda." Nami nikasema, "Mimi—mimi nakuomba umsaidie."

147 Na nilipokuwa nikiomba, nilisikia Kitu kinasema, "Simama kwa miguu yako." Nami niliendelea katika kuomba, maana ni—ni—nilidhani kuwa nimeliwaza hilo. Nami nilipoendelea kuomba, Kitu fulani kikasema, "Simama kwa miguu yako." Nami nikaacha kuomba, na kuangalia juu. Na picha ya Kristo, ile ambayo . . .

148 Kamwe sikutia maanani picha ya Sallman. Mimi—mimi napenda picha ya Hofmann, *Kichwa cha Mtu wa Miaka Thelathini na Mitatu*, mnajua. Nami ninayo picha kubwa aina hiyo, sababu, wakati nilipomwona Yeye katika ono wakati ule, Yeye alionekana namna hiyo. Nayo ilikuwa pale, nimeitundika kwa namna ambayo Yeye angekuwa akinitazama wakati nikiomba, katika picha hii.

149 Nami nilitazama juu pale, na nikaitazama ile picha. Na nikatazama kila mahali. Nikafikiri, "Ilikuwa ni kitu gani, 'Simama kwa miguu yako'?" Nikawaza, "Vema, nitasimama kwa miguu yangu." Nami nikasimama kwa miguu yangu.

150 Ni Sauti ile ile iliyonena pale juu ya kilima usiku ule, Yeye yule Ambaye siku zote anakuja. Nikasema, "Bwana Mungu, huyo alikuwa ni Wewe unazungumza na mtumishi Wako?"

151 Alinena, "Sema neno tu, na hapatakuwa na uvimbe tena."

152 Nilisimama pale kitambo kidogo, kujiweka sawa. Wengi wenu mnajua, hapa, na watu wa Maskani wanajua ilikuwa kitu gani, alichokuwa nacho. Nilisema, "Basi nasema, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, kwamba huo uvimbe utamuacha." Ulikuwa ukimsumbua mno, hata kwamba alikuwa kitandani kwa siku tatu au nne, kwa ajili yake. Nikasema, "Hawataona kamwe hata alama yake. Kwa maana, Bwana Mungu wangu, ambaye ni Muumbaji, ambaye anaweza kusimamisha upepo na dhoruba, na anaweza kuzikemea bahari, na kutenda hili, Yeye ni Muumba wa mbingu na nchi. Nami nampenda Yeye na kumuamini Yeye, nami naamini kwamba wakati huu unakaribia wakati

mambo haya yatatendeka. Na Wewe, ambaye uliweza kuumba kindi na kumfanya awepo, unaweza kumwondolea mbali adui." Nikasema, "Wakati Ibilisi alipoingia katika dhoruba . . . Upepo ni kiumbe cha Mungu. Maji ni kiumbe cha Mungu. Bali Ibilisi alijiingiza humo, hiyo ndiyo ilisababisha mambo hayo, na kutia yale—yale machafuko katika bahari, jinsi hiyo." Nikasema, "Wewe uliweza kuituliza. Na Wewe uliyeweza kuituliza hiyo, unaweza kuondoa uvimbe kutoka kwa mke wangu. Nami nasema kwamba limetendeka sasa hivi, huo hautaonekana kamwe. Umekwisha."

153 Nilitoka pale na uhakika, nikamwambia mwanangu na mke wa mwanangu. Tukaja hapa, na usiku uliopita nilikuja humu mbio kufanya mkutano; na nikarudi, nikampigia simu. Naye alikuwa bado hajafahamu lolote kuhusu jambo hili. Sikumwambia.

154 Na wakati aliponipigia simu, alikuwa amejaa furaha. Akasema, "Billy, nataka kukwambia jambo fulani, mpenzi." Akasema, "Hakuna alama hata moja ya uvimbe iliyosalia popote. Daktari alisema kwamba hakuona lolote." Akasema, "Nilifurahi sana! Na Bi. Norman na dada wengi hapa, wawili au watatu kati yao, walikuwa pamoja nasi hapa chumbani." Akasema, "Daktari alisema, 'Na wataka kusema! Sielewi. Mwezi mmoja uliopita, kulikuwa na uvimbe pale ukubwa wa balungi.' Na akasema, 'Bi. Branham, nakuhakikishia, huna alama hata moja ya uvimbe po pote juu yako." Daktari wake angalijua mahali ulipokuwa.

155 Ni Bwana Mungu wetu! Je ni siku ya shukrani? Loo, Mungu ashukuriwe kwa kipawa cha Yesu Kristo, hicho Kipawa kikuu ambacho ni yeye yule jana, leo, na hata milele! Hiyo ni kweli. Siamini kujiapiza kwa mbingu juu, au cho chote kile. Bali Biblia ikiwa kifuani mwangu, na Mungu Ambaye nampenda, anajua kwamba kila neno la hayo ni kweli kabisa. Siku ya Shukrani! Wakati nilikuwa nikiwaza kuwa kesho ningeweza au siku chache zijazo, huenda ingalinilazimu hata kuacha mkutano, niende. Sikuweza hata kuwaahidi watu kwamba ningerudi wakati wa Krismasi, kule nyumbani, kwa ajili ya watoto wangu, kuwarudisha nyumbani tena kwa wakati wa Krismasi; nikijua, na kutetemeka ndani ya moyo wangu, kwamba upasuaji ulimngojea mke wangu, akiwa na uvimbe wa ukubwa wa balungi. Na ulikuwapo pale.

156 Na lile Neno la Mungu, lililonena, "Sema utakalo, nalo litakuwa hivyo."

157 Nami nilisema, "Uvimbe umekwisha. Hawatauona tena."

158 Na huo umekwisha, leo. Na wataalamu wa upasuaji walio wazuri sana na madaktari wazuri sana walikuwa kule Tucson, Arizona; wakati, siku chache zilizopita, kulikuwa na uvimbe mkubwa, mkubwa sana namna *hiyo*. Na daktari yule yule

hakuweza kuona alama yake kamwe, na aliandika taarifa namna hii, kwamba, "Bi Branham hana alama ya uvimbe, mahali popote."

159 Loo, shukrani kwa Mungu! Hii ni siku ya kutoa shukrani, kwangu mimi. Kujua, zaidi ya hilo, kwamba siku moja huo uso mdogo niliouoa kule, atukuzwe Mungu, siku moja alama hizi za kifo za uzeeni zitatoweka, na tutakuwa kule mfano wa ujana, na hatutazeeka kamwe. Na karama ya Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo, ya Roho Mtakatifu ambayo tumepokea sasa, ndiyo inatupa hii, hii nanga.

160 Na iangalie hiyo leo, marafiki. Nyinyi mnazungumza kuhusu watu walio na shukrani, sisi tunapaswa kuwa watu wenye shukrani sana zaidi ya wote katika ulimwengu! Mbali na uponyaji, mbali na mambo haya yanayotendeka, ni kitu gani? Ni uhakika kamili kwamba Mungu yule yule, kwa tabia ile ile, Nguzo ya Moto ile ile, Malaika wa Mungu yule yule, Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele, amefanya mambo yale yale, kwa Nguvu zile zile, anafanya jambo lile lile. Ni nanga jinsi gani ya nafsi iliyo imara na hakika! Bwana Mungu wa Mbinguni awabariki sana, kila mmoja.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

161 Bwana, ninashukuru sana, Bwana, mimi—mimi sijui hata la kusema. Hata siwezi kufafanua jambo hili. Wakati huo wimbo ulipoimbwa muda mfupi uliopita, na hao watu waliouimba huo wimbo, moyo wangu ulirukaruka kwa furaha. Na ushuhuda ukaja kwenye moyo wangu. Na sasa, Baba wa Mbinguni, Wewe unajua mambo haya ni kweli. Wewe unajua, kutoka kilindi cha moyo wangu, hayo, na kwamba hayo ni kweli. Sina sababu, Bwana, kuwaeleza lolote isipokuwa lile ambalo ni kweli. Nami naomba, Mungu, kwamba leo. . . moyo wangu ujisikie kuwaona hawa ndugu wote pamoja na dada Wakristo walioko hapa, ambao ni ndugu zangu na dada zangu katika kifungo cha Kristo, wakishangilia pamoja nami, pamoja na shukrani, kwa ajili maskini mwenzangu [Mahali patupu kwenye ukanda—Mh.] amehifadhiwa. [Mahali patupu kwenye ukanda] . . . dunia na inasifu Mungu. Hebu maumbile na yamsifu Mungu! Hebu vyote vyenye pumzi, vimsifu Mungu na kushukuru kwa ajili ya huu wakati mkuu tulio nao.

162 Mpendwa Baba wa Mbinguni, pale naona kuna mvulana mdogo amekaa hapa katika kiti cha kusukumia wagonjwa. Kuna wengine hapa ambao ni wagonjwa na wahitaji. Na kama Wewe ulivyo Mungu wa wokovu wa nafsi zetu, Wewe ni Mungu ambaye huponya magonjwa yetu yote na mateso yetu. Na Wewe bado . . . pamoja na hizi shuhuda, moja tu au mbili, ambapo zinafikia maelfu, ambazo mtumishi Wako mnyenyekevu ameona Wewe ukifanya na kutenda, pasipo waa hata moja ndani yake, popote. Nasi tunajua kwamba Wewe bado ni Yehova - Yire, na Wewe

tayari umekwishatoa Dhabihu kwa ajili ya uponyaji. Mungu yule hasa ambaye aliondoa ule uvimbe katika ubavu wa mke wangu, Wewe ni Mungu uliyepo hapa Shreveport kama tu vile ulivyokuwa kule Tucson; na bado nilikuwa maili kadha, maili elfu mbili kutoka kwake wakati huo. Naomba, Mungu, kwamba Uwepo Wako Mtakatifu utaijaza hii Maskani leo, kwa Nguvu za uponyaji, ambazo zitamponya kila mgonjwa aliyeko hapa, kwamba hizi baraka za shukrani ziendelee kusikika, huku na kule, kote nchini, Bwana, kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Jalia hili, Mungu wa Milele.

163 Sasa enyi watu mnaoketi hapa, wekeni mikono yenu mmoja juu ya mwingine na kuomba. Jiunganisheni wenyewe pamoja kwa umoja wa imani katika Uwepo wa Mungu, na kumbukeni kwamba kila mmoja wenu ametunukiwa. Mungu atanihukumu, iwapo nimewaambia ukweli au la. Je liliwahi kubatilika, nimewahi kuwaambia jambo lolote isipokuwa lile ambalo lilitukia?

164 Kama Samweli alivyosema wakati ule, kama wakati walikuwa wanakwenda kumfanya awe—awe mfalme, Sauli. Alisema, "Je nimewahi kuwaambia jambo lolote katika Jina la Bwana, isipokuwa lile lilitokea? Je niliwahi kuwaomba pesa zenu, kwa ajili ya chakula changu?" "Hapana, Samweli, lakini sisi bado tunataka mfalme. Sisi bado tunataka mfalme wetu wa duniani." Na Samweli alijua kwamba Mungu alikuwa ndiye Mfalme wao.

165 Nawaambia, asubuhi ya leo, enyi watu, nataka mshuhudie, je mmewahi kuona karama ya Mungu ikishindwa hata wakati mmoja, ambayo tumesoma habari zake asubuhi ya leo? Hapana, bwana. Ni Yesu Kristo, haiwezi kushindwa. Sayansi imethibitisha hilo. Kanisa linajua hilo. Na Yeye yuko hapa sasa hivi, dakika hii. Yuko hapa. Na kitu pekee kinachopungua ni imani yako kuchukua hilo Neno na kujipatia upako Wake, na Yeye atakuponya.

166 Na huku mkiwekeleana mikono nyinyi kwa nyinyi, mlilie Mungu, kwa moyo wako wote, na kusema, "Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, Wewe Ambaye unaweza kuituliza dhoruba, miaka elfu mbili iliyopita, Wewe ulifanya hivyo na unafanya hivyo tena sasa hivi. Na Wewe hukomesha kuugua kwangu. Hunifanya niwe mzima. Nami nakushukuru moyoni mwangu, Mwenyezi Mungu. Amina.

USHUHUDA SWA63-1128M
(Testimony)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi asubuhi, Novemba 28, 1963, katika Maskani ya Uzima kule Shreveport, Louisiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1990 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org